88122388

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Thursday 15 November 2012 (afternoon)
Jeudi 15 novembre 2012 (après-midi)
Jueves 15 de noviembre de 2012 (tarde)

1 h 30 m

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.



© International Baccalaureate Organization 2012

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

## Toleo Maalum

# SEKTA YA UZALISHAJI VIWANDANI NA BIDHAA ZA WALAJI



Sekta ya uzalishaji bidhaa za viwanda na walaji imekuwa ikibadilika kwa miaka kadhaa ulimwenguni kote Tanzania ikiwemo huku suala la bidhaa zenye kujali mazingira likizingatiwa. Pengine kwa mara ya kwanza sekta ya habari kupitia kwa magazeti yako yanayoongoza The Guardian na Nipashe yatakuletea Toleo Maalum Sekta ya Uzalishaji viwandani na bidhaa za walaji zenye kuzingatia mazingira tarehe 31 Julai 2012.

Miongoni mwa mada zitakazomulikwa katika toleo hilo ni pamoja na: Ni vipi wazalishaji na viwanda Tanzania wanavyozingatia dhana hii ya "Bidhaa rafiki kwa mazingira", ushirikiano wa wenye viwanda na Serikali na Mamlaka zake, ufahamu wa walaji juu ya dhana hii na nyingine nyingi.

Makala hizi zote zitaandikwa na wataalum waliobobea.

Tafadhali mpendwa mtangazaji na wadau kama vile watengenezaji na wauzaji wa mashine za viyoyozi na mifumo ya kupooza hewa watengenezaji na wauzaji rangi ya majumba, wazalishaji wa vifaa vya ujenzi, benki zenye kutambulisha sera za za mazingira, viwanda vya sementi bila kuwasahau wasambazji mafuta na mitambo ya magari, viwanda vya karatasi, maji ya kunywa na vifaa vya plastiki na wengine wengi wa bidhaa za viwanda na walaji.

Kushiriki kwa kuweka tangazo lako la biashara kutakupa fursa ya kipekee ya kuandikiwa makala yako bure.


Kutoka *Nipashe*, Julai 2012



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

# Ndoa na mapenzi



Nakumbuka ilikuwa desturi ya Zawadi kwenda maziarani alikozikwa mchumba wake Rashid. Aliwahi kwenda huko mara nyingi sana na Amina. Siku moja alipitia kwangu chumbani wakati wa jioni na mafungu ya mchanga mkononi. Akanisihi tuandamane pamoja. Tulipofika maziarani akayaweka mafungu hayo ya mchanga kwenye kaburi la Rashid. Akanyamaza kwa kitambo kirefu, machozi yakimtoka. Akakitoa kitambaa pochini na kuyafuta machozi. Zawadi akanishika mkono ghafla na kunielekeza kwa upembe mwingine wa maziara. Hapo tukaketi kitako.

"Zilikuwa zimesalia siku tatu tu," alisema Zawadi. "Baada ya hizo siku tatu ningeolewa. Halafu Rashid akanitupa mkono. Najua hayakuwa. Mapenzi yake. Lakini sikuamini kwamba amekufa. Sikutaka kuolewa na mwanamume yeyote mwingine. Lakini upweke umenizidia. Sidhani nitaendelea kuwa hivi nilivyo. Nataka kuolewa kama wanawake wengine niondokane na ukiwa."

"Marahaba," niliitikia. "Kama wataka kuolewa vema. Hata mimi nilidhani ilifaa sana kwako kupata mume wa kukuoa. Pengine hawezi kuwa muungwana kama Rashid. Lakini Mungu hamnyimi mja wake yote. Ingawa umemkosa Rashid utapewa mwingine pindi utakapo."

"Lakini wajua," akasema Zawadi, "Shida iliyopo ni kwamba mwanamke anaweza kuvutika na mtu na kumdondokea lakini asiweze kujijasirisha kumwambia kuwa anampenda mtu huyo. Hiyo ndiyo dhiki yenyewe. Katika Afrika si kawaida mwanamke kumuuliza mwanamume kuanza mambo ya mahaba na ndoa. Unamtamani mtu, ila huna uso wa kumkabili na kumwambia nakupenda."

"Ee! Wasemaje Zawadi?"

"Mimi nina haya," akajibu. "Hata nikimpenda mtu nashindwa kumwambia."

"Kwani umempenda mtu ukashindwa kumwambia?" Nikamuuliza.

"Ndiyo," akajibu.

"Nani huyo?" nikauliza tena.

"Wewe. Nakupenda sana. Nataka unioe."

Nilighumiwa kwa muda. Nilipoangalia uso wa zawadi nikaona kuwa hayakuwa masihara bali mazingatio. Niliona kuwa umri wangu wa miaka kumi na sita wakati huo haukutosha kunivumilisha masaibu yaliyomo katika ndoa. Aidha wazo la kumuoa mchumba wa rafiki yangu ingawa alishakufa zamani lilinipa msito nikasita. Zawadi alikuwa msichana mzuri wa umbo na tabia. Haikuwa sahili kukataa katakata ombi lake. Nilitafuta kila njia ya kujinasua kutoka kwa mtego ulioninasa.

"Mimi sikufai wewe Zawadi," nilimwambia baada ya kuwaza kwa muda. "Nitizame uzuri. Umri wangu bado mdogo mno. Tena nilimpenda sana marehemu Rashid."

"Hilo si neno," alinena Zawadi. "Mapenzi ni kama mgomba, popote hujiotea."

"Lakini mgomba changaraweni haupandwi ukamea," nikasema.

Kutoka *Siku Njema* na Ken Walibora



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

# TUWAHESHIMU WAKUU WETU



Tangu jadi, jambo la kimbele alilofunzwa mtoto ni kuwaheshimu wakubwa. Siku hizo ukubwa ulihusishwa na umri. Ilibidi kila mwanajamii kumheshimu yeyote aliyemzidi kwa umri. Heshima ilifikia kilele kwa wazee. Iliaminika kuwa uzee ni hidaya. Kadiri mtu alivyokomaa kiumri, ndivyo alivyopanua mzingiro wake wa tajriba, busara na hekima. Vitambulisho vingine vya uzee vilikuwa pamoja na mvi kichwani, mikunjo usoni na upara. Katika baadhi ya jamii, kigoda na mavazi au mapambo maalum vilitumiwa kuwatambulisha waliostahili kuheshimiwa. Utii haukubagua mume au mke. Ole wako kama hukuwatii wazee! Kizazi chako chote kililaaniwa. Utii ni jambo la jamii zote ukimwenguni. Hata vitabu vya dini mbalimbali husistiza utii kwa wakubwa.

Vigezo vinavyotumiwa kuongoza utii vimebadilika siku hizi. Ingawa umri bado unatumiwa, kigezo muhimu zaidi ni madaraka. Mamlaka aliyo nayo mtu hutegemea elimu, tajriba, hekima na wakati mwingine mali anayomiliki. Kwa hivyo, yeyote anayeshikilia wadhifa fulani uwe katika utumishi wa umma, shirika, dini, chama, jeshi, shule au mkutano, hana budi kutiiwa. Hoja hii inaandamana na hekima ya methali “akikalia kigoda basi mtii”. Ukweli wa kauli hii unabainika kupitia uwezekano siku hizi wa kupata mkurugenzi wa kampuni mwenye umri wa miaka ishirini na mitano tu huku kaimu wake akiwa mzee wa mika hamsini na kitu.

Tatizo ni kuwa siku hizi watu hawazingatii kito hiki muhimu. Vijana hasa hawawaheshimu wala kuwatii watu wanaowazidi umri. Vijana wa kileo hawajali wazee. Na kama mzee hakusoma au hakuvaa vizuri, anadharauliwa kweli. Mzee akiwa mwanamke ndio basi vijana husahau kuwa mwana mtukana nina kuzimu enda kiona.

Mwelekeo huu ni hatari. Ni lazima urekebishwe. Hii ni kwa sababu jamii inayoheshimu wakuu huneemeka. Jamii isiyotii wakubwa nayo hupata kinyume chake ambacho ni balaa. Lakini kwanza lazima tujiulize, kama kuwaheshimu ni kufanya nini?

Kwanza, ni kuwasatahi. Yaani kuwatia maanani na kujali kuwepo kwao. Tunapowataka radhi na kuwaendea wakati wa shida badala ya kujiamulia mambo, basi tunawaheshimu. Pili ni kuwatii. Inapasa wadogo watekeleze kulingana na amri matakwa na mapenzi ya wakubwa, kukaidi na kupuuza watakavyo au kuwafanyia kiburi ni kutowaheshimu.

Tangu utotoni, tunajua kuwa heshima si utumwa. Moja ya sifa za heshima ni kuwajali wakubwa. Huku ni kujitolea kuwahudumia na kuwatendea inavyostahili. Ni vizuri kuwapisha tuseme njiani au wakati wa chakula. Si heshima kushindana nao au kuwapiga kumbo. Kitendo kingine cha heshima ni kuwanyenyekea. Yapasa uhusiano wetu nao uwe wa adabu. Ni adabu njema kuwaamukua kwa taadhima. Ajabu ni kuwa siku hizi neno shikamoo limesahaulika. Heshima inadai lugha ya adabu, kuzingatia itifaki na kutumia anuani zinazotambulisha vyeo vya wakuu. Rais atajwe kwa kwa anuani Mtukufu, Kadinali, Mwadhama. Anuani kama Profesa, Daktari, Mama, Mzee, n.k. zote zitumiwe ipasavyo.

Kwa hivyo, tunapowahujumu, kutusi, kusengenya na kudharau wakuu, basi tunatenda kinyume na mahitaji ya heshima. Hata hivyo heshima si uhewala. Si vizuri kuwaabudu na kuwasujudia wakuu; yaani haifai kuwacha wakuu kiasi cha kuogopa kuwakosoa na kutetemeka mbele yao na kutekeleza kila wanachoamuru hata kama ni kibaya. Tuna wajibu kuwapinga lakini tufanyavyo hivyo tutumie lugha ya adabu.

Halikadhalika wazee hutuasa kuwa mwenye kutenda jamala naye hulipwa jamala. Wakuu nao wanawajibika kujiheshimu na kuwaheshimu wadogo wao. Mkuu anayewatendea wema na haki wadogo wake huweka msingi imara wa heshima.

Kutoka *Kiswahili Fasaha*, Francis Waititu et al.



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# HOTUBA

Hamjambo wananchi.



Nimefurahi jinsi mlivyofika kwa wingi; wakubwa kwa wadogo. Bila kupoteza wakati, ningependa kuwambia kwamba mimi ninaitwa Juma Makanga. Mimi ni mtoto wenu kutoka katika kijiji hiki cha Nyangeli.

Nimewaita ili kuwajulisha kwamba ningependa kuwa mbunge wenu. Tafadhali nipeni nafasi ili niweze kuwaakilisha bungeni na ninawahakikishia kwamba hamtajuta. Eneo hili la bunge limesalia nyuma sana upande wa maendeleo. Haya yote yanatokana na ile hali ya kuwachagua viongozi ambao hawajimudu. Wengi hutudanganya kwamba wtatufanyia mengi tukiwachagua; ajabu ni kwamba wanapofika bungeni wao huyaweka yale waliyotuahidi katika buku la sahau.

Ningependa kuwahakikishia kuwa nitakuwa mtumishi wenu. Mkinichagua, nitawaafanyia mengi. Barabara zote katika eneo hili la bunge zitawekwa lami. Hamtakuwa na matatizo ya kusafiri wala kusafirisha bidhaa zenu.

Wananchi watukufu, kuna watoto wengi sana katika maeneo haya ambao hupita mtihani wao wa darasa la nanevizuri lakini huwa hawaendelei na masomo. Ukata umeua ndoto za vijana wengi sana. Mkinichagua, nitaanzisha mradi wa kuwaelemisha watoto maskini ambao no werevu. Nyakati za kuua ndoto za kuwa madaktari na mawakili wa baadaye umekwisha.

Ndugu zangu, uhalifu umekithiri mipaka katika sehemu zote za eneo hili. Watu wanishi kwa uoga sana. Kuna vijana ambao wanazururazurura ovyoovyo na kuwavamia watu kuanzia saa moja za jioni. Mkinichagua, wakizurura ovyoovyo watatiwa ndani.

Pombe haramu imevunja nyumba nyingi sana. Wanaume wengi hawarudi nyumbani, wamepotelea katika anasa. Isitoshe kuna vifo vingiambavyo husababishwa na pombe haramu. Hivi juzi kuna wazee watano ambao walikunywapombe haramu na wakawa vipofu. Nitapiga marufuku unywaji wa pombe haramu ili tuwe na taifa lililosimama imara la wafanyakazi.

Tafadhali nipeni fursa hii ili muweze kunijaribu. Ikiwa sitawaakilisha vizuri, basi tafadhali mniite nirudi nyumbani na muweze kuchagua kiongozi mwingine wa vitendo. Kwa hivyo, utakapoenda kwenye kituo cha kupiga kura, usisahau kumpigia Juma Makanga. Ishara yangu ni kidole cha gumba.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Kutoka *Johari ya Kiswahili*, Collins et al.



https://xtremepape.rs/